# HALMASHAURI YA MJI MASASI

## MJI WETU-FAHARI YETU

Jarida la Mtandaoni | *Toleo na. 03* | *www. masasitc.go.tz* | Januari-Machi 2024

## YALIYOMO


▶Zijue Fursa za Mji wa Masasi, Kitovu cha Biashara Mkoa wa Mtwara



Michezo Uk..15

Makala Uk..13

▶Baraza la Madiwani lapitisha rasimu ya Bajeti ya bilioni 30.1

▶Maafisa ugani kanda ya kusini wapigwa msasa.

▶Kamati ya Fedha na Utawala yakagua utekelezaji wa miradi

▶Mafunzo ya mfumo wa mama na mwana yatolewa Masasi.

▶Rc Mtwara akabidhi Madawati 1500 Mji Masasi.

▶Jamii iendelee kushiriki kikamilifu kampeni za chanjo.

▶Dc Kanoni azindua kliniki ya kusikiliza kero za wananchi.

▶"Sukari Masasi iuzwe kwa Bei elekezi", Dc Kanoni.


*Tembelea Tovuti yetu kupata Nakala yako/www.masasitc.go.tz*


"Skani kusoma"

©Halmashauri ya Mji Masasi

# ZIJUE FURSA ZA MJI WA MASASI, KITOVU CHA BIASHARA MKOA WA MTWARA

Halmashauri ya Mji Masasi ni **kitovu cha biashara** ndani ya Mkoa wa Mtwara. Mji huu umeshamiri fursa mbalimbali za uwekezaji ukipendezeshwa na masoko ya bidhaa, viwanda, hoteli na viwanja vya uwekezaji.


Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Masasi




## ZIJUE KATA ZA HALMASHAURI YA MJI MASASI

MASASI MJI

| | |
|---|---|
| MKUTI | JIDA |
| MKOMAINDO | MIGONGO |
| NAPUPA | TEMEKE |
| NYASA | MUMBAKA |
| MTANDI | MWENGEMTAPIKA |
| CHANIKANGUO | MATAWALE |
| SULULU | MARIKA |


Barabara Kuu kutoka Mataa(Standi) kwenda Tunduru

Mji huu upo kilomita 210 kusini magharibi mwa mkoa wa Mtwara, ukiwa na ukub wa wa hekta 37,920 huku idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi 2022 ikiwa ni watu 137,585 wanaume wakiwa 65,781 na wanawake 71,804.

Mji huu unafikika kwa urahisi kutoka pande zote za nchi kwani ni makutano makuu ya Miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa mizigo/bidhaa kutoka na kwenda wilaya nyingine ndani ya mkoa na mikoa mingine kama Ruvuma, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

Ni makutano ya barabara kuu za Tunduru- Songea-Mbeya, Lindi-Mtwara-Dar es salaam,Nachingwea-Liwale pamoja na Newala-Tandahimba.Shughuli kuu za kiuchumi kwa wakazi wa Mji wa Masasi ni Kilimo na Biashara.Mazao yanayolimwa kwa wingi ni korosho, ufuta,mbaazi na mazao mbalimbali.

Inaendelea Uk...3

Hali ya hewa, Mji huu hupata mvua za wastani kati ya milimeta 900-1000 kwa mwaka.Kipindi cha mvua ni kuanzia mwezi Novemba hadi April. Wastani wa nyuzi joto kipindi cha mvua ni sentigrade 25.

Ni Mji pekee unaokua kibishara kusini mwa Tanzania.Hii ni **Masasi Mpya** kama ilivyo **falsafa ya Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini** Mhe. Geoffrey Mwambe.

Akieleza fursa za Masasi Mji mbele ya maelfu ya wananchi waliojitokeza katika mkutano wa hadhara wa Rais Mhe, Dkt Samia Suluhu Hassan uliofanyika katika uwanja wa boma Masasi mjini Septemba 17, 2023, Mhe Mwambe alisema Masasi ni Mji wa uwekezaji,uliofunguka kwenye huduma muhimu za kijamii kuanzia afya, maji, barabara za lami, elimu,biashara, kilimo na umeme.

"Mhe.Rais nakushukuru sana kwa kung'arisha Masasi, Mji unang'aa Mji ni mpya barabara za lami ziko nyingi na zinapendeza..." alisema Mhe Mwambe.

Huu ndio upekee wa **"Kariakoo ya Mtwara"**kama alivyobainisha **Mkuu** wa Wilaya **ya Masasi** Mhe. Lauter John Kanoni wakati akiwatambulisha viongozi akiwemo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba sambamba na Mkurugenzi wa Mji Masasi katika mkutano wa hadhara wa Rais Dkt Samia.

"Mji huu wa Masasi ni mji wa kibiashara, hapa ni katikati ya maeneo yote, halmas hauri zote zinakuja kutafuta mahitaji yao hapa, kariakoo yao ni hapa" alisema Mhe Kanoni.

**Mwenyekiti wa Halmashauri** ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba anasema Masasi ni **Kitovu cha Biashara, hivyo anawakaribisha wawekezaji kuwekeza Masasi Mji.** Kutokana na Fursa, upatikanaji wa huduma za maji, umeme na mawasiliano ya simu na mtandao, miundombinu ya barabara, Uwepo wa ardhi ya kutosha na hali ya hewa kwaajili ya ustawishaji wa mazao ya biashara, Huduma za kijamii,shule za kutosha za michepuo ya kingereza na kiswahili,Vituo vya kutolea huduma za afya vya kisasa na masoko ya bidhaa yanapatikana.



Mhe. Hashim Namtumba
Mwenyekiti Halmashauri ya Mji Masasi

> *Halmashauri ya Mji Masasi ni kitovu cha biashara Mkoa wa Mtwara.Huu ni Mji unaoendelea kwa kasi sana. Fursa za uwekezaji zimeshamiri,Kazi kubwa inayofanywa na Wah. Madiwani imeonekana na kwakweli tunamshukuru Mhe Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe Geoffrey Mwambe kwani Masasi mpya imewezekana na kiupekee Rais wetu, Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.*

**Mkurugenzi wa Mji Masasi,** Ndg Reuben Jichabu anasema Upatikanaji wa vibali vya **shughuli za uwekezaji ni rahisi** unapohitaji kuwekeza Halmashauri ya Mji Masasi. Anasema mazingira ya uwezeshaji, utatuzi wa changamoto, elimu ya fursa, maeneo ya uwekezaji na viwanja vya makazi na biashara vinapatikana kwa urahisi na haraka.

# BARAZA LA MADIWANI MJI MASASI LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 30.1 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.



Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe Hashim Namtumba na Mkurugenzi wa Mji Ndg. Reuben Sixbert Jichabu (kulia)


Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe.Geoffrey Mwambe na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe, Hamisi Nikwanya (Kulia)


Mkuu wa divisheni ya Mipango na Uratibu Mji Masasi, Ndg. Prosper Luambano (akiwasilisha)


Waheshimiwa Madiwani wakiwa katika mkutano wa baraza la bajeti

Baraza la Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi limejadili na kuidhinisha rasimu ya mapendezo ya mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo Halmashauri hiyo inakadiria kupokea na kutumia jumla ya Tsh. 30,195,139,106.07.

Akizungumza katika mkutano wa Baraza la Madiwani la kujadili na kupitisha bajeti hiyo Februari 29, 2024,Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba amesema bajeti hiyo imezingatia mapendezo yote muhimu ya waheshimiwa madiwani na hivyo itakwenda kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wa Masasi Mji.

Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe amesema bajeti hiyo imezingatia vipaumbele vya wananchi wa Masasi Mji.

Amesema mbali na bajeti hiyo bado anaendelea kupambana kwa dhati kuhakikisha ujenzi wa masasi mpya unawafikia wananchi wa Masasi Mji katika kata zote 14 kupitia uboreshaji wa miundombinu ambapo barabara ya kisasa yenye miradi funganishi kama stendi ya kisasa inakwenda kujengwa sambamba na maboresho ya kisasa katika standi ya uwanja wa fisi (ambayo ameshauri maboresho yakishafanywa jina libadilishwe), sambamba na ujenzi na maboresho katika eneo la Sokosela.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu amesema katika jitihada za kuongeza mapato ya ndani, katika mwaka wa fedha 2024/2025 wanatarajia kujenga hoteli ya kisasa yenye kumbi kubwa tatu za mikutano na kumbi ya starehe sambamba na kuboresha miundombinu ya shule, kuwezesha wananchi kiuchumi, kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya.

Akiwasilisha rasimu ya bajeti hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mji, Mkuu wa divisheni ya Mipango na Uratibu Halmashauri ya Mji Masasi, Ndg. Prosper Luambano amesema Halmashauri inakadiria kupokea na kutumia jumla ya shilingi 30,195,139,106.07 kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Amesema vyanzo hivyo ni mapato ya ndani shilingi 3,397,212,700.00, matumizi mengineyo shilingi 1,040,957,000.00, Mishahara-shilingi 18,764,926,000.00, Miradi ya maendeleo (Serikali kuu na Wahisani) shilingi 6,992,043,406.07

Amesema vipaumbele vya bajeti hiyo ni kuongeza mapato ya ndani kutoka Tshs 2.8 Billion ya sasa hadi Tshs Billioni 3.4., Kuimarisha shughuli za utawala bora, Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya,Uimarishaji wa usafi wa mazingira, Kuboresha miundombinu ya shule za Msingi, Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Ukamilishaji wa miradi viporo na Umilikishaji.

# KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA YAKAGUA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.

Kamati ya fedha na Utawala Halmashauri ya Mji Masasi Januari 25, 2024 imetembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.



Kamati hiyo imeongozwa na Makamu Mwenyekiti Halmashauri Mhe, Hamisi Nikwanya akimwakili sha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe Hashim Namtumba.

Kamati hiyo imetembelea na kukagua Ujenzi wa vyumba vya madarasa, Matundu ya vyoo na bwalo Shule ya Sekondari Mwengemtapika, Ujenzi wa Jengo la upasuaji hospitali ya Mkomain do, Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Mkomain do, shule mpya ya Msingi Darajani,shule ya msingi mkomaindo na shule mpya ya sekondari Jida.

Kamati pia imekagua Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Jida unaotekelezwa kwa fedha za Sequip kwa gharama ya Tsh. 560,552,872.



Jengo la upasuaji Hospitali ya Mkomaindo (Mapato ya ndani)



Shule ya Msingi Darajani (Mradi wa Boost)

Aidha imekagua Ujenzi wa Vyumba 9 vya madarasa na Matundu 16 ya vyoo vya Shule ya Msingi Mkomaindo unaotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha Tsh. 208,000,000.

Pia imetembelea na kukagua Ujenzi wa Bwalo, Madarasa na Vyoo shule ya Sekondari Mwengemtapika unao tekelezwa na fedha kutoka Serikali Kuu kwa gharama ya Tsh 320,000,000.



Shule mpya ya sekondari Jida (Mradi wa Sequip).

Kamati hiyo imepongeza juhudi za Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Mhe. Geoffrey Mwambe kwa jitihada za kuhakikisha miradi inawafikia wananchi wa Masasi Mji sambamba na kutoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

# RC MTWARA AKABIDHI MADAWATI 1500 HALMASHAURI MJI MASASI. ASEMA NI REKODI YAKISTORIA





Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema Halmashauri ya Mji Masasi imeweka rekodi kubwa na ya kihistoria kwa kutengeneza jumla ya mada wati 1500 yenye thamani ya Tsh 112,500, 000 kwa ajili ya kutatua changamoto ya madawati kwa shule za awali na msingi.

Aidha amewapongeza, Waheshimiwa Madiwani, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Mkuu wa Wila ya na Mkurugenzi wa Mji Masasi kwa jitihada za kuhakikisha madawatihayo yanatengenezwa.

Kanali Ahmed Abbas amesema hayo Januari 31, 2024 wakati akikabidhi madawati hayo katika hafla iliyofanyika katika viunga vya shule ya sekondari ya Wasichana Masasi.

“Leo nimekuja kushuhudia jambo kubwa na lakihistoria ambalo kwakweli mmeweka rekodi nzuri, ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati nikiwa na furaha kubwa sana, kwa halmashauri ya Mji Masasi kwa kutengeneza madawati 1500. Napenda kuwapon geza waheshimiwa madiwani na Mkurugenzi wa Mji Masasi kwa jitihada kubwa mliyo ifanya katika kuondoa tatizo la madawati kwa shule ya msingi na nimpongeze sana Mwakilishi wa Wananchi Mhe, Mbunge wa Jimbo Hili la Masasi Mjini, Mhe Geoffrey Mwambe kwa ushirikiano mzuri na Halmashauri hii ya Mji, na Ushirikiano Mzuri na Serikali kwa kuhakikisha haya yanatokea, lakini pia pongezi zangu ni kwa Mhe. Rais Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha tunakuwa na miundombinu ya kisasa ya kutolea elimu, shule mpya zimejengwa, madarasa mapya na miundombinu mingi kwenye sekta hii imejengwa”

Awali, akitoa ripoti ya utengenezaji wa madawati hayo, Mkurugenzi wa Mji Masasi, Ndg. Reuben Sixbert Jichabu amesema, Idara ya elimu ya awali na msingi ina jumla ya wanafunzi 25, 328 kati yao wavulana 12555 na wasichana 12773 ambapo mahitaji ya madawati yalikuwa 8443 na yaliyokuwepo ni madawati 6552 na upungufu ulikuwa ni 1891.

Amesema mkakati wa awali ulikuwa ni kukarabati madawati yote mabovu kwenye shule za awali na msingi ambapo madawati 225 yamekarabatiwa na Halmashauri imefanikiwa kutengeneza madawati 1500 yenye thamani ya Tsh 112, 500,000/= ambayo yatagawiwa katika shule 31 za awali na msingi na kituo shikizi.

# DC KANONI AZINDUA KLINIKI YA KUSIKILIZA NA KUTATUA KERO ZA WANANCHI MASASI.



Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni Machi 7, 2024 amezindua rasmi kliniki ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi wa Wilaya Masasi.

Amesema zoezi hilo alilolizindua katika mkutano uliofanyika katika eneo la Uwanja wa Fisi, Halmashauri ya Mji Masasi litafanyika katika Kata zote za Wilaya ya Masasi, ambapo wananchi watapata nafasi ya kutoa kero zao na kupatiwa utatuzi wa papo kwa papo

“Leo ni siku ya kliniki sio ile ya hospitali tupo kwenye kliniki ya kusikiliza kero, changa moto na kuzitatua, tumekuja kuwasikiliza wananchi, tumezindua na tutakwenda kata kwa kata, tumeanza na Halmashauri ya Mji Masasi tutakwenda pia Halmashauri ya Wilaya”. Dc kanoni

Amesema Serikali imeendelea kuhakikisha huduma katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi, miundombinu zinaboreshwa huku akimpongeza Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe kwa juhudi zake za kuhakikisha changamoto mbalimbali zinatatuliwa ikiwemo ujenzi wa barabara za kisasa, ujenzi wa standi mpya, maji, kusai dia watoto wanaotoka katika mazingira magumu kwenda shule kwa kubainisha kuwa hizo zote ni dhamira zake za dhati katika kuijenga Masasi mpya.

Diwani kata ya Napupa Mhe. Sospeter Nachunga amesema zoezi hilo ni muhimu na lina maslahi mapana kwa maendeleo ya wananchi wa Masasi na amewasihi wananchi kuitumia fursa ya kliniki hiyo kuzungumza kero zote na si kwenda kuzungumza pembe ni kwani majibu ya changamoto zote yanapatikana katika mikutano hiyo.

Wakizungumza mara baada ya utatuzi wa kero mbalimbali, wananchi wamepongeza hatua hiyo ya kuwafikia moja kwa moja katika mikutano ya wazi na kuomba kliniki hiyo iendelee kuwafikia wananchi katika maeneo yote ya Wilaya ya Masasi.

Inaendelea Uk...8

Uzinduzi wa kliniki hiyo umehudhuriwa na Mhe Diwani Kata ya Napupa, Kaimu Mkuru genzi wa Mji, Wakuu wa Idara na Vitengo, Viongozi wa Taasisi zote za Serikali zikiwemo Nida, Manawasa, Tarura, Tanesco, Kamati ya ulinzi na usalama na wananchi wamepa ta suluhu ya kero mbalimbali.

Tangu uzinduzi wa kliniki hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Masasi amesikiliza na kutatua kero za wananchi wa kata za Matawale na Sululu kwa Halmashauri ya Mji Masasi huku akiendelea kwenye kata mbalimbali zilizobakia.

## MAAFISA UGANI KANDA YA KUSINI WAPIGWA MSASA





Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi leo Machi 21, 2024 imeendelea na zoezi la kuwanoa maafisa ugani wa sekta ya Mifugo waliopo kanda ya kusini inayojumuisha mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye mafunzo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Jengo la Utawala, Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter Kanoni amewasisitiza maafisa ugani hao kuhakikisha wanatumia mafunzo hayo kwenda kubadili mfumo wa ufugaji kutoka ule wa holela hadi ufugaji wa kisasa.

“Wakati wa msimu wa mvua hali ni shwari lakini ikifika kiangazi sisi na nyie Maafisa Mifugo huwa hatulali kila kukicha tunaenda kushughulikia migogoro baina ya wakulima na wafugaji hivyo tumieni mafunzo haya kuwabadili wafugaji waanze kufuga kisasa ili kuepusha madhara baina ya pande hizo mbili” Amesisitiza Mhe. Kanoni.

Aidha Mhe. Kanoni amewataka watalaam hao katika sekta ya Mifugo kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa chanjo kwa mifugo ili kuepusha madhara kwa mifugo na watumiaji wa mazao ya Mifugo hiyo.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Maafisa Ugani wenzake, Daktari wa Mifugo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Bi. Subira Simbeye ameahidi kwenda kutekeleza maele kezo yote yaliyotolewa na Mhe. Kanoni ili kuendelea kuboresha sekta ya Mifugo kwa mikoa ya Lindi na Mtwara.

Inaendelea Uk...9

Awali akiwasilisha mada ya “Sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma”, Afisa Utumishi Mwandamizi kutoka Wizarani hapo Bi. Suzan Silayo amewata ka Maafisa ugani hao Kufanya kazi kwa uadilifu, kuzingatia maadili ya utumishi na kufuata sheria kanuni na taratibu za kiutumishi.

“Pia mkafanye kazi bila upendeleo na muwe waaminifu wakati wote huku mkitoa ushauri kwa viongozi wenu pale inapobidi kwa kuwa wao nyie ndio wataalamu lakini wakati wote msisahau kutunza siri za serikali” Ameongeza Bi. Silayo

Aidha Bi. Silayo amewataka wataalam hao kuepuka kutoa au kupokea rushwa huku pia akiwasisitiza kujiandaa na maisha ya baada ya kustaafu katika Utumishi wa Umma kwa kuhakikisha wanafanya uwezekaji wa kutosha pindi wakiwa kazini.

Mafunzo hayo kwa Maafisa Ugani wa mikoa ya kanda ya Kusini yatafanyika kwa siku 2 ambapo mada mbalimbali zinatarajiwa kuwasilishwa kwa wataalam hao kwa lengo la kuwakumbuka taratibu mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yao pindi wakiwa uwandani.

## “SUKARI MASASI IUZWE KWA BEI ELEKEZI ISIYOZIDI TSH 3200” DC KANONI.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni amewataka wafanyabiashara kuwa waaminifu kwa kuhakikisha wanauza sukari kwa bei elekezi ya Serikali ambayo ni 3200/= kwa kilo moja ya Sukari.



Mhe Kanoni ametoa agizo hilo Machi 01, 2024 wakati wa mapokezi ya shehena ya sukari zaidi ya tani mia moja katika eneo la Jida (Tandale ya zamani) Halmashauri ya Mji Masasi.

Amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea na jitihada mbali mbali za kuhakikisha wananchi wanapata sukari ya kutosha kwa bei elekezi.

“ Tumepokea Shehena ya sukari ya kutosha, sitegemei kuona kuanzia leo, Machi 01, 2024 mfanyabiashara yeyote kuwa atauza sukari kinyume na bei elekezi, na bei elekezi ya Serikali kwa kilo moja ya sukari haizidi Tsh.3200/= na hii ni katika Wilaya yote ya Masasi na mkoa wa Mtwara. Kiupekee Masasi tumepata mzigo huu zaidi ya tani 100. Naagiza kuwa Mwananchi yeyote utayemkuta mfanyabiashara anakuuzia sukari zaidi ya bei elekezi, toa taarifa haraka ili hatua za kisheria zichukuliwe. Adhabu ni kutaifisha mzigo wote wa sukari, kufungiwa leseni yako ya biashara na kufikishwa mahakamani” Dc

Inaendelea Uk...10

Wafanyabiashara wa jumla wamemhakikisha Mkuu wa Wilaya kwamba watauza sukari kwa bei elekezi ambayokwa kilo 50 ni Tsh 140,000 na kilombero sukari kilo 25 ni Tsh 75,000.

Mapokezi ya shehena ya sukari hiyo yameshuhudiwa na Mkurugenzi wa Mji Masasi, wananchi, wafanyabiashara wa jumla na rejareja, kamati ya ulinzi na usalama na wakuu wa Idara na vitengo na viongozi mbalimbali kutoka Serikali za mitaa.

## MAFUNZO YA MFUMO WA MAMA NA MWANA YATOLEWA HALMASHAURI YA MJI MASASI.





Katibu Tawala wilaya ya Masasi Bi. Fatima Kubenea kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya amewataka washiriki wa mafunzo ya mfumo wa mama na mwana kuhakikisha wanazingatia mafunzo hayo ili kwenda kuboresha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa mama na mtoto.

Amesema hayo Februari 23, 2024 wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Mfumo wa Mama na Mwana kwa watendaji wa vijiji, wahudumu wa afya ngazi ya jamii (WAJA) na watoa huduma za afya Halmashauri ya Mji Masasi.

Amesema Mfumo wa utoaji mrejesho utakwenda kuboresha huduma ya Mama na mwana na kuleta ufanisi kwa watoa huduma za afya.

Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji Masasi, Ndg. Benjamin Shilinde amesema Mfumo huu ni mahususi kwa ajili ya kupata maoni ili kuboresha huduma ya afya ya uzazi na Walengwa wa mpango huo ni mama mjamzito, mama mwenye mtoto chini ya umri wa mwezi mmoja.

Amesema walengwa watajiunga katika mfumo huo kwa kutumia simu yeyote kwa kujisajili na kuandika neno MAMA kwenda namba 15077 bure na ataulizwa ubora wa huduma alioupata katika kituo alichohudhuria.

# JAMII IENDELEE KUSHIRIKI KIKAMILIFU CHANJO YA SURUA NA RUBELLA





Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni amewataka wazazi kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kampeni ya Chanjo ya Surua na Rubella kwa kuwapeleka watoto kupata chanjo hiyo muhimu inayotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na maeneo mbalimbali yaliyoandaliwa.

" Nichukue fursa hii kuwatangazia wananchi wa Masasi kushiriki kikamilifu zoezi hili kwa kuwapeleka watoto kwenye vituo vya afya na maeneo mengine yaliyoandaliwa ili watoto wakapate chanjo bure bila malipo yoyote" Mkuu wa Wilaya Mhe. Kanoni.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya Mji Masasi ambaye pia ni diwani kata ya Mkomaindo, Mhe Ally Salvatory akizindua chanjo hiyo Februari 15 alisema ushiriki wa jamii ulioneshwa katika chanjo hiyo unapaswa kuendelezwa katika chanjo zote.

"Kwa maelezo ya wataalamu kutoka ngazi ya mkoa ni kwamba Masasi Mji hatujawahi kufeli kwenye mazoezi ya chanjo, tunafanya vizuri, mwitikio ni mkubwa sana,tuendelee kuwa mabalozi wazuri wa chanjo"

Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi Ndg. Andrea Kalinga amesema watoa huduma katika vituo kutolea huduma za afya na maeneo yaliyoandaliwa wapo tayari kutoa huduma ya chanjo ya Surua na Rubella kwa watoto wenye miezi kuanzia tisa hadi chini ya miaka mitano.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Masasi Dkt. Salum Gembe amesema Ofisi ya Rais- Tamisemi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wameandaa Kampeni ya Chanjo ya Surua na Rubella kwa watoto walio chini ya miezi tisa mpaka chini ya miaka mitano.

Kampeni hiyo imefanyika kuanzia tarehe 15- 18 Februari 2024 katika vituo vya kutolea huduma za afya Halmashauri ya Mji Masasi na maeneo mbalimbali yaliyoandaliwa.

Alisema Jumla ya watoa huduma 50 kutoka katika vituo 20 vinavyotoa huduma ya chanjo wamepata mafunzo hayo muhimu.Amesema walengwa watarajiwa ni watoto 12,091 wenye miezi 9 hadi 59.

# "HATA BILA SARE NJOO SHULE, SERIKALI HAIJAWEKA KIKWAZO CHOCHOTE" DC KANONI.





Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni Januari 9, 2023 ametembelea na kukagua zoezi la uripoti wa wanafunzi katika shule za Msingi na sekondari katika Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.

Mhe. Kanoni ametembelea shule za msingi mbalimbali ikiwemo darajani, Mtandi na Mkuti B na shule za sekondari mbalimbali ikiwemo Anna Abdallah, Jida sekondari, Mtandi na shule ya kutwa Masasi ( Masasi Day) kwa ajili ya kufuatilia uripoti wa shule za msingi na kidato cha kwanza.

Katika ziara hiyo, amewapongeza wazazi kwa kuhakikisha wanafunzi wa awali wanaripoti shuleni kwa asilimia 100.

"Kwa upande wa shule za Msingi kwa wanafunzi wa awali kwa Halmashauri yetu ya Mji wa Masasi kwa shule ambazo tumezikagua uripoti wa wanafunzi ni asilimia 100, wanafunzi wote waliokuwa wameandikishwa wamesharipoti, kwa upande wa darasa la kwanza wastani ni asilimia 80, kwahiyo maendeleo kwa siku hizi mbili tupo vizuri", Dc Kanoni.

Mhe, Kanoni amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaweka mazingira mazuri na bora ya kuwawezesha wanafunzi wa awali, darasa la kwanza na shule za msingi na sekondari kwa kuhakikisha wanasoma katika mazingira mazuri.

Aidha amewataka wazazi kuhakikisha wanaendelea kuwapeleka watoto shule kwa kuwa hakuna kikwazo chochote cha kutowapeleka wanafunzi shuleni kwani hata bila sare wanapokelewa na kuanza masomo.

# MAKALA

**KUTOKANA NA KASI KUBWA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KAA TAYARI KUSOMA “JARIDA MAALUMU LA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO” KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024, UTAKALOLIPATA HIVI KARIBUNI.**



Ndg. Reuben Sixbert Jichabu
Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi

“Kama waheshimiwa madiwani mnavyokumbuka kwenye bajeti hii tunayotekeleza (2023/2024) tulitenga fedha kwaajili ya kumalizia miradi mbalimbali ikiwemo kumalizia shule ya sekondari Temeke, tayari fedha yake tumeshaikusanya,ipo tayari. inapofikia mwisho wa mwezi wa sita miradi yote itakuwa imekamilika. Lengo ni kuhakikisha miradi iliyotengwa kwenye bajeti tunaitekeleza na kuikamilisha yote.”



**ELIMU KWA MLIPAKODI**

# LIPA USHURU

## NA LESENI

## KWA MAENDELEO YA

## HALMASHAURI YA MJI MASASI



## “MJI WETU, FAHARI YETU”

*Elimu kwa mlipakodi*

**Wasiliana nasi.**
Mkurugenzi wa Mji Masasi
Anuani ya Posta: P.o.box 447, Masasi
Simu ya Mezani: +255232510685
Barua pepe: info@masasitc.go.tz
Tovuti: www.masasitc.go.tz
Fb, Insta, Twitter (X), Youtube: halmashauri mji masasi

# MICHEZO

## VIPAJI VYA MICHEZO MASASI KUUZWA KITAIFA NA KIMATAIFA





Klabu ya Azam FC yenye maskani yake Jijini Dar es Salaam imeingia mkataba na kituo cha Maendeleo youth sports center kutoka Masasi kwaajili ya ushirikiano wa kuuza wachezaji katika soko la ndani na nje ya Nchi.

Mkataba huo umetiwa saini Machi 11, 2024 kati ya Kampuni ya Azam na Maendeleo youth sports center ambacho ni kituo cha kuibua na kukuza vipaji vya watoto na vijana kuanzia miaka 9 na kuendelea kikiwa kimesajiliwa mwaka 2014 kwa namba NS 12377.

Katika kuimarisha ushirikiano huo, Timu ya masoko ya kampuni ya Azam ilitembelea kituo hicho tarehe 12/04/2024 na kuongea na wachezaji na viongozi wa kituo hicho wakiongozwa na Mkurugenzi wa ufundi, Kizito Mbano na Kocha Hamisi Omary Dulaz.

Ushirikiano huo ni fursa muhimu kwa vijana wenye vipaji vya michezo kutoka Masasi kujitangaza na kuuza vipaji katika masoko ya kitaifa na kimataifa ambavyo vitachangia kwenye kuinua uchumi wa familia, vijana na Serikali.



Mwenyekiti wa Halmashaur ya Mji Masasi Mhe Hashim Namtumba akikabidhi zawadi ya Jezi seti moja kwa klabu ya Stand Fc baada ya kutwaa Ubingwa wa soka Mkoa wa Mtwara.



Mbunge Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe katika kukuza na kuendeleza michezo Machi 3, 2024 aligawa jezi kwa timu za mpira wa miguu Masasi.

# MATUKIO KATIKA PICHA




Halmashauri ya Mji Masasi imezindua kampeni ya kupanda miti Februari 14, 2024, Miti 500,000 kupandwa



Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi wakijadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa miradi.



Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu akizungumza katika Mkutano wa hadhara kata ya Sululu



Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi wakishuhudia zoezi la kukabidhi madawati 1500 shuleni.

Jarida la Mtandaoni limeandaliwa na,
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Mji Masasi